TANGAZO LA SERIKALI NA. 353 la tarehe 10/05/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA VIWANDA MBEZI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Viwanda Mbezi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji(mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango

3. Mipango kina katika eneo lililotajwa chini ya aya 2 itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SF874 yenye majira - nukta 521852.302MS, 9259238.835KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SF875 yenye majira - nukta 521932.482MS,

*Tangazo La Serikali Na. 353 (Linaendelea)*

9259304.116KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.07 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SF912 yenye majira - nukta 521982.399MS, 9259245.18KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SF911 yenye majira - nukta 521900.907MS, 9259181.398KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.07 hadi ulipoanzia".

Dodoma — JERRY WILLIAM SILAA

25 April, 2024 — *Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*